Policy Brief: TZ.11/2010K

# Je, Waliwajibika?

## Tathmini ya miaka mitano ya Bunge 2005-2010





### 1. Utangulizi

Tarehe 16 Julai mwaka 2010, baada ya kikao cha 20 cha Bunge, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alivunja Bunge la 9. Tukio hili liliashiria mwisho wa muhula wa Wabunge waliochaguliwa katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2005. Kwa kuwa kikao cha mwisho kimeshamalizika, tunapata fursa ya kutazama nyuma na kuangalia utendaji wa wabunge wakati wa muda wao. Je, walishiriki kikamilifu na kuwakilisha majimbo yao kwa kuuliza maswali na kuchangia hoja ama walikaa kimya?

Bunge ni chombo kikuu cha kupitisha sheria Tanzania. Bunge linatoa idhini ya fedha kutumika kwa ajili ya kuendesha utawala na kusimamia mipango ya serikali. Bunge linasimamia utendaji kazi wa Serikali Kuu na hutumika kama jicho la kuhakikisha kuwa Serikali inawajibika kwa wananchi wake. Ili kufanikisha yote haya, Wabunge wanapitisha sheria, wanaidhinisha kodi na kuchunguza sera, pamoja na mapendekezo ya matumizi ya Serikali; na hujadili masuala muhimu ya kila siku. Ili Bunge liweze kufanya kazi yake ya usimamizi vizuri, ushiriki hai wa wabunge ni muhimu. Wabunge wanaweza kushiriki kwa namna tatu: wanaweza kuuliza maswali ya msingi, kuuliza maswali ya nyongeza, au kuchangia hoja wakati wa mijadala.

Muhtasari huu ni muendelezo wa ile iliyotangulia, wa mwisho ulitolewa mwezi Agosti mwaka 2010. Muhtasari huu unawasilisha mambo saba kuhusu ushiriki wa Wabunge, ikiwa ni pamoja na kuonesha wabunge wenye kuongoza kwa ushiriki na wale wenye ushiriki mdogo.

Taarifa zilizotumika katika muhtasari huu zimepakuliwa kutoka kwenye POLIS (Parliamentary On-line Information System) iliyopo kwenye tovuti ya Bunge (http://www.bunge.go.tz) Mwezi Agosti 2010. Aidha data kamili zinaweza pia kupakuliwa kutoka kwenye tovuti ya Uwazi (www.uwazi.org).

Uwazi
pata picha kamili

Taarifa hii imetolewa na Uwazi iliyopo Twaweza/Hivos Tanzania.

Uwazi, S.L.P 38342, Dar es Salaam, Tanzania.
Simu +255 22 266 4301. Nukushi +255 22 266 4308.
Barua pepe: info@uwazi.org. Tovuti: www.uwazi.org

Kimetolewa Oktoba 2010


## 2. Mambo saba makuu kuhusu Bunge 2005-2010

Ili kuweza kutathmini utendaji wa wabunge katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, tunawasilisha ripoti ya wabunge wote 322: 231 waliochaguliwa, 75 wa viti maalum, 10 wa kuteuliwa na Rais, 5 kutoka Baraza la Wawakilishi la Zanzibar na Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Katika baadhi ya sehemu za taarifa hii tunatofautisha wabunge ambao ni wajumbe wa Baraza la Mawaziri na wale ambao si wajumbe wa Baraza hilo. Katika sehemu ambazo utofautisho unafanywa kwa njia hii, tunakuwa tumeweka bayana.

### Jambo la kwanza: CCM ni chama kinachochangia zaidi Bungeni

Jumla ya idadi ya ushiriki wa wabunge ni 25,765 katika vikao 20 vya Bunge kukiwa na wastani wa michango 80 kwa kila mbunge. CCM inaongoza kwa michango ya ushiriki 21,196, ikifuatiwa na CUF kwa michango ya ushiriki 2,713, CHADEMA ikitoa michango ya ushiriki 1,647, na UDP 209. Wabunge wa CCM kuchangia zaidi si jambo la kustaajabisha kwa kuwa wabunge 278 (asilimia 86 ya wabunge wote) ni wa CCM, wakati 32 (asilimia 10) ni wa CUF, 11 (asilimia 3) ni wa CHADEMA, na mmoja (asilimia 0.3) ni wa UDP.

**Kielelezo na. 1: Ushiriki Bungeni ki-chama**





**Chanzo:** Tovuti ya Bunge (www.bunge.go.tz).

### Jambo la pili: Wabunge wa CCM walikuwa na ushiriki mdogo zaidi Bungeni

Kielelezo namba 2 kinaonesha utendaji wa vyama mbali mbali kwa kutathmini wastani wa ushiriki  kwa kila mbunge. Kwa maswali ya msingi CHADEMA inaongoza kwa wastani wa maswali 20 kwa kila mbunge. CHADEMA pia inaongoza katika kuuliza maswali ya nyongeza ikiwa na wastani wa maswali ya nyongeza 40 kwa kila mbunge. UDP yenye Mbunge mmoja, ndiyo imeongoza katika kuchangia hoja. Chama tawala kimekuwa cha mwisho katika kuuliza maswali ya nyongeza. CUF ni cha mwisho katika kutoa michango, ikitoa wastani wa michango 48 kwa kila mbunge wakati UDP hakikuuliza swali la msingi hata moja.

Tukizingatia jumla ya idadi ya ushiriki, CCM ni ya mwisho ikiwa na wastani wa ushiriki wa 76 kwa kila mbunge, ikifuatiwa na CUF (85), CHADEMA (150) na UDP (209).

**Kielelezo na. 2: Wastani wa idadi ya maswali na michango kwa kila mbunge, ki-chama**





**Chanzo:** Tovuti ya Bunge la Tanzania (www.bunge.go.tz).

## Jambo la tatu: Wabunge wa kuchaguliwa wanashiriki zaidi

Kielelezo namba 3 kinaonesha Wabunge wa kuchaguliwa ndio wanaongoza kwa ushiriki katika vipengele vyote vitatu (maswali ya msingi, maswali ya nyongeza na michango). Wabunge kutoka Baraza la Wawakilishi la Zanzibar pamoja na wale wa kuteuliwa na Rais ndio wenye ushiriki mdogo zaidi katika vikao vya Bunge. Zingatia kwamba kipengele hiki hakimjumuishi Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**Kielelezo na. 3: Wastani wa ushiriki wa Wabunge, kwa-aina ya ubunge**





**Chanzo***:* Tovuti ya Bunge la Tanzania (www.bunge.go.tz).

## Jambo la nne: Wabunge wanaume wanashiriki zaidi

Bunge la 9 la Tanzania lina Wabunge wa kiume wapatao 222, na wa kike wapatao 100. Kama ilivyooneshwa katika kielelezo namba 4, katika vipengele vyote vitatu wastani wa ushiriki wa Wabunge wa kiume ulizidi ule wa Wabunge wanawake kwa kiasi kidogo.

**Kielelezo na. 4: Wastani wa ushiriki wa Wabunge, kwa jinsia**





**Chanzo**: Tovuti ya Bunge la Tanzania (www.bunge.go.tz).

## Jambo la tano: Mawaziri wana ushiriki mdogo Bungeni

Bunge lina jumla ya wajumbe wa Baraza la Mawaziri 48 wakiwemo: Mawaziri 26, Naibu Waziri 21, na Waziri Mkuu. Wote hawa ni Wabunge wa CCM. Kati ya hawa, 41 hawakuwahi kuuliza swali hata moja la msingi katika kipindi chote cha miaka mitano Bungeni.

Kati ya wabunge 267 wasio wajumbe wa Baraza la Mawaziri ama viongozi wa ngazi za juu Serikalini (tukijumuisha (naibu) Spika na Makamishna wa Mkoa), wabunge 39 hawakuuliza swali hata moja la msingi.

**Kielelezo na. 5: Maswali ya msingi yaliyoulizwa na Mawaziri na Wabunge wa kawaida**




**Chanzo:** Tovuti ya Bunge la Tanzania (www.bunge.go.tz).

## Jambo la sita: Mheshimiwa Ndugai ndiye anayeongoza kwa ushiriki bungeni

Ili kutambua ushiriki wa wabunge kwa ujumla, hususan wasio kuwa wajumbe kwenye Baraza la Mawaziri, wasio Makamishna wa Mkoa ama Spika na Naibu wake, aina tatu ya ushiriki ilijumuishwa. Ujumuishwaji ulifanyika kwa kutizama ni mara ngapi Mbunge aliweza kuuliza maswali ya msingi, maswali ya nyongeza, na kuchangia hoja.

Kigezo hiki kinapotumika, Mh. Ndugai ndiye mwenye kuongoza kwa ushiriki akiwa ameshiriki mara 376: yakiwemo maswali ya msingi 29, maswali ya nyongeza 60 na akichangia hoja mara 287. Mbunge anaye fuatia kwa ushiriki ni Mh. Jenista Mhagama akifuatiwa na Mh. Wilbrod Slaa, Mh. Godfrey Zambi na Mh. Zitto Kabwe.

**Jedwali na 1: Wabunge wanaoongoza kwa ushiriki Bungeni**


| |  |  |  |  |  |
|---|---|---|---|---|---|
| | Job Yustino Ndugai | Jenista J. Mhagama | Dr.Wilbrod P. Slaa | Godfrey W. Zambi | Kabwe Z. Zitto |
| | CCM | CCM | CHADEMA | CCM | CHADEMA |
| Nafasi | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| Jumla | 376 | 364 | 284 | 265 | 261 |
| Kuchangia hoja | 287 | 275 | 159 | 163 | 180 |
| Maswali nyongeza | 60 | 63 | 103 | 69 | 56 |
| Maswali ya msingi | 29 | 26 | 22 | 33 | 25 |

**Chanzo:** Tovuti ya Bunge la Tanzania (www.bunge.go.tz).

## Jambo la saba: Mheshimiwa Aziz ndio Mbunge mwenye ushiriki mdogo zaidi

Kwa kutumia kigezo kilekile kilichotumika kwenye jambo la 6, imeonekana kuwa Mh. Rostam Aziz wa CCM ndiye Mbunge mwenye ushiriki mdogo zaidi kati ya wabunge wa 'kawaida'. Mh Aziz ndiye mbunge pekee ambaye hakuchangia kwa namna yoyote ile katika kipindi chake chote cha miaka mitano bungeni. Wabunge wengine wenye ushriki mdogo ni Mh. Ali Suleiman, Mh Ali Ali, Mh. Salum Salum, na Mh Yusuf Makamba.

**Jedwali Na. 2: Wabunge walioshiriki kwa uchache zaidi Bungeni.**

| |  |  |  |  |  |
|---|---|---|---|---|---|
| | Rostam A. Aziz | Ali H. Suleiman | Ali H. Ali | Salum K. Salum | Col.Lt.Yusuf Makamba |
| | CCM | CCM | CCM | CCM | CCM |
| Nafasi | 267 | 266 | 265 | 264 | 263 |
| Jumla | 0 | 2 | 4 | 4 | 4 |
| Kuchangia hoja | 0 | 1 | 4 | 4 | 4 |
| Maswali ya nyongeza | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Maswali ya msingi | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |

**Chanzo**: Tovuti ya Bunge la Tanzania (www.bunge.go.tz).

## 3. Hitimisho

Taarifa hii imetumia taarifa huru zinazopatikana kwenye tovuti ya Bunge la Tanzania ili kutathmini ushiriki wa wabunge katika vikao 20 vya Bunge la 9 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kati ya mwaka 2005 na 2010.

Imebainika kuwa Wabunge wamepishana sana katika ushiriki. Mh. Ndugai ndiye mwenye ushiriki wa juu zaidi akiwa na jumla ya ushiriki wa mara 379. Mbunge mwenye ushiriki mdogo zaidi ni Mh. Azizi ambaye hakuuliza swali wala kutoa mchango wowote Bungeni. Bila shaka, idadi ya ushiriki ni kiashiria kimojawapo tu cha utendaji kazi wa Mbunge. Majukumu mengine ni kufanya kazi kwenye Kamati za Bunge, na ushiriki kwa wananchi majimboni mwao. Hata hivyo, taarifa hii inawapa wananchi mtazamo muhimu wa kutathmini ni kwa jinsi gani Wabunge wamefanya kazi kwa ajili ya maslahi ya wananchi. Taarifa hii pia inatoa fursa kwa kila chama cha siasa na kwa kila Mbunge kufafanua zaidi ni kwa namna gani wamekuwa wakitumika kwa maslahi ya majimbo yao katika kipindi cha miaka mitano. Mijadala ya wazi ya namna hii ni muhimu kwa kukuza demokrasia, na uwajibikaji.

**Kiambatanisho na.1: Nafasi ya Ushiriki wa Wabunge (Wabunge wasio na Nyadhifa muhimu Serikalini)**

| Nafasi | Jina | Jinsia | Chama | Jimbo | Maswali ya msingi | Maswali ya nyongeza | Michango | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Job Yustino Ndugai | Me | CCM | Kongwa | 29 | 60 | 287 | 376 |
| 2 | Jenista Joakim Mhagama | Ke | CCM | Peramiho | 26 | 63 | 275 | 364 |
| 3 | Dr. Wilbrod Peter Slaa | Me | CHADEMA | Karatu | 22 | 103 | 159 | 284 |
| 4 | Godfrey Weston Zambi | Me | CCM | Mbozi Mashariki | 33 | 69 | 163 | 265 |
| 5 | Kabwe Zuberi Zitto | Me | CHADEMA | Kigoma Kaskazini | 25 | 56 | 180 | 261 |
| 6 | Diana Mkumbo Chilolo | Ke | CCM | Hana jimbo | 41 | 88 | 120 | 249 |
| 7 | Mgana Izumbe Msindai | Me | CCM | Iramba Mashariki | 44 | 94 | 99 | 237 |
| 8 | George Malima Lubeleje | Me | CCM | Mpwapwa | 34 | 87 | 112 | 233 |
| 9 | Juma Hassan Killimbah | Me | CCM | Iramba Magharibi | 26 | 66 | 134 | 226 |
| 10 | Susan Anselm Jerome Lyimo | Ke | CHADEMA | Hana jimbo | 23 | 46 | 146 | 215 |
| 11 | John Momose Cheyo | Me | UDP | Bariadi Mashariki | 0 | 24 | 185 | 209 |
| 12 | William Hezekia Shellukindo | Me | CCM | Bumbuli | 40 | 59 | 108 | 207 |
| 13 | Siraju Juma Kaboyonga | Me | CCM | Tabora Mjini | 27 | 47 | 126 | 200 |
| 14 | Said Amour Arfi | Me | CHADEMA | Mpanda Kati | 26 | 69 | 104 | 199 |
| 15 | Prof. Raphael Benedict Mwalyosi | Me | CCM | Ludewa | 32 | 58 | 103 | 193 |
| 16 | Mohamed Habib Juma Mnyaa | Me | CUF | Mkanyageni | 15 | 69 | 102 | 186 |
| 17 | Magdalena Hamis Sakaya | Ke | CUF | Hana | 22 | 46 | 117 | 185 |
| 18 | Hamad Rashid Mohamed | Me | CUF | Wawi | 18 | 90 | 72 | 180 |
| 19 | Salim Hemed Khamis | Me | CUF | Chambani | 26 | 56 | 95 | 177 |
| 20 | Lucy Fidelis Owenya | Ke | CHADEMA | Hana | 29 | 43 | 99 | 171 |
| 21 | John Paul Lwanji | Me | CCM | Manyoni Magharibi | 30 | 30 | 109 | 169 |
| 22 | Michael Lekule Laizer | Me | CCM | Longido | 29 | 65 | 74 | 168 |
| 23 | Stella Martin Manyanya | Ke | CCM | Hana | 17 | 30 | 114 | 161 |
| 24 | Mohamed Rished Abdallah | Me | CCM | Pangani | 25 | 87 | 49 | 161 |
| 25 | Lucas Lumambo Selelii | Me | CCM | Nzega | 29 | 58 | 73 | 160 |
| 26 | Zubeir Ali Maulid | Me | CCM | Kwamtipura | 9 | 26 | 114 | 149 |
| 27 | Bujiku Philip Sakila | Me | CCM | Kwimba | 22 | 31 | 95 | 148 |
| 28 | Emmanuel Jumanne Luhahula | Me | CCM | Bukombe | 30 | 45 | 71 | 146 |
| 29 | Mhonga Said Ruhwanya | Ke | CHADEMA | Hana | 30 | 41 | 74 | 145 |
| 30 | Esther Kabadi Nyawazwa | Ke | CCM | Hana | 20 | 72 | 52 | 144 |
| 31 | Ruth Blasio Msafiri | Ke | CCM | Muleba Kaskazini | 20 | 28 | 92 | 140 |

| Nafasi | Jina | Jinsia | Chama | Jimbo | Maswali ya msingi | Maswali ya nyongeza | Michango | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 32 | Herbert James Mntangi | Me | CCM | Muheza | 34 | 33 | 71 | 138 |
| 33 | George Boniface Simbachawene | Me | CCM | Kibakwe | 24 | 55 | 57 | 136 |
| 34 | Vita Rashid Kawawa | Me | CCM | Namtumbo | 25 | 55 | 55 | 135 |
| 35 | Benson Mwailugula Mpesya | Me | CCM | Mbeya Mjini | 28 | 42 | 63 | 133 |
| 36 | Aloyce Bent Kimaro | Me | CCM | Vunjo | 24 | 48 | 61 | 133 |
| 37 | Raynald Alfons Mrope | Me | CCM | Masasi | 24 | 47 | 58 | 129 |
| 38 | Paul Peter Kimiti | Me | CCM | Sumbawanga Mjini | 24 | 24 | 79 | 127 |
| 39 | Hafidh Ali Tahir | Me | CCM | Dimani | 25 | 68 | 34 | 127 |
| 40 | Savelina Silvanus Mwijage | Ke | CUF | Hana | 22 | 26 | 78 | 126 |
| 41 | Fuya Godwin Kimbita | Me | CCM | Hai | 21 | 29 | 75 | 125 |
| 42 | Martha Mosses Mlata | Ke | CCM | Hana | 14 | 32 | 79 | 125 |
| 43 | Dr. Chrisant Majiyatanga Mzindakaya | Me | CCM | Kwela | 27 | 47 | 50 | 124 |
| 44 | Castor Raphael Ligallama | Me | CCM | Kilombero | 24 | 24 | 76 | 124 |
| 45 | Mohamed Hamisi Missanga | Me | CCM | Singida Kusini | 17 | 26 | 80 | 123 |
| 46 | Omar Shabani Kwaangw' | Me | CCM | Babati Mashariki | 19 | 24 | 78 | 121 |
| 47 | Halima James Mdee | Ke | CHADEMA | Hana | 26 | 30 | 64 | 120 |
| 48 | Paschal Constantine Degera | Me | CCM | Kondoa South | 36 | 37 | 46 | 119 |
| 49 | Mussa Azan Zungu | Me | CCM | Ilala | 23 | 35 | 59 | 117 |
| 50 | Khalifa Suleiman Khalifa | Me | CUF | Gando | 20 | 57 | 39 | 116 |
| 51 | Andrew John Chenge | Me | CCM | Bariadi Magharibi | 0 | 0 | 116 | 116 |
| 52 | Felix Ntibenda Kijiko | Me | CCM | Muhambwe | 22 | 20 | 72 | 114 |
| 53 | Mwanne Ismaily Mchemba | Ke | CCM | Hana | 19 | 33 | 61 | 113 |
| 54 | Gosbert Begumisa Blandes | Me | CCM | Karagwe | 28 | 25 | 60 | 113 |
| 55 | Stanley Jilaoneka Yono Kevela | Me | CCM | Njombe Magharibi | 23 | 27 | 62 | 112 |
| 56 | Ponsiano Damiano Nyami | Me | CCM | Nkasi | 22 | 54 | 36 | 112 |
| 57 | Jacob Dalali Shibiliti | Me | CCM | Misungwi | 25 | 25 | 62 | 112 |
| 58 | Faida Mohamed Bakar | Ke | CCM | Hana | 23 | 57 | 31 | 111 |
| 59 | Mkiwa Adam Kimwanga | Ke | CUF | Hana | 18 | 22 | 67 | 107 |
| 60 | Pindi Hazara Chana | Ke | CCM | Hana | 25 | 12 | 69 | 106 |
| 61 | Daniel Nicodem Nsanzugwanko | Me | CCM | Kasulu East | 11 | 15 | 79 | 105 |
| 62 | Prof. Idris Ali Mtulia | Me | CCM | Rufiji | 15 | 15 | 75 | 105 |
| 63 | James Daudi Lembeli | Me | CCM | Kahama | 26 | 40 | 38 | 104 |
| 64 | Mbaruk Kassim Mwandoro | Me | CCM | Mkinga | 27 | 23 | 52 | 102 |

| Nafasi | Jina | Jinsia | Chama | Jimbo | Maswali ya msingi | Maswali ya nyongeza | Michango | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 65 | Mgeni Jadi Kadika | Ke | CUF | Hana | 30 | 24 | 47 | 101 |
| 66 | Mwanawetu Said | Ke | CUF | Hana | 12 | 29 | 59 | 100 |
| 67 | Dr. Guido Gorogolio Sigonda | Me | CCM | Songwe | 22 | 17 | 61 | 100 |
| 68 | Clemence Beatus Lyamba | Me | CCM | Mikumi | 19 | 17 | 63 | 99 |
| 69 | Masolwa Cosmas Masolwa | Me | CCM | Bububu | 29 | 20 | 50 | 99 |
| 70 | Mwadini Abbas Jecha | Me | CUF | Wete | 17 | 17 | 65 | 99 |
| 71 | Ania Said Chaurembo | Ke | CUF | Hana | 24 | 31 | 43 | 98 |
| 72 | Peter Joseph Serukamba | Me | CCM | Kigoma Mjini | 12 | 26 | 60 | 98 |
| 73 | Fatma Abdallah Mikidadi | Ke | CCM | Hana | 13 | 24 | 60 | 97 |
| 74 | Shoka Khamis Juma | Me | CUF | Micheweni | 28 | 26 | 42 | 96 |
| 75 | Charles N. Keenja | Me | CCM | Ubungo | 22 | 19 | 54 | 95 |
| 76 | Nuru Awadhi Bafadhili | Ke | CUF | Hana | 15 | 26 | 53 | 94 |
| 77 | Sijapata Fadhili Nkayamba | Ke | CCM | Hana | 23 | 30 | 41 | 94 |
| 78 | Riziki Omar Juma | Ke | CUF | Hana | 21 | 27 | 46 | 94 |
| 79 | Dr. Luka Jelas Siyame | Me | CCM | Mbozi Magharibi | 12 | 16 | 66 | 94 |
| 80 | Victor Kilasile Mwambalaswa | Me | CCM | Lupa | 32 | 24 | 38 | 94 |
| 81 | Dr. Raphael Masunga Chegeni | Me | CCM | Busega | 20 | 36 | 38 | 94 |
| 82 | Dr. Harrison George Mwakyembe | Me | CCM | Kyela | 14 | 16 | 63 | 93 |
| 83 | Zaynab Matitu Vulu | Ke | CCM | Hana | 6 | 27 | 59 | 92 |
| 84 | Anne Kilango Malecela | Ke | CCM | Same Mashariki | 24 | 36 | 32 | 92 |
| 85 | Vedastusi Mathayo Manyinyi | Me | CCM | Musoma Mjini | 15 | 26 | 51 | 92 |
| 86 | Vuai Abdallah Khamis | Me | CCM | Magogoni | 18 | 16 | 57 | 91 |
| 87 | Dr. Binilith Satano Mahenge | Me | CCM | Makete | 16 | 25 | 50 | 91 |
| 88 | Dr. Samson Ferdinand Mpanda | Me | CCM | Kilwa Kaskazini | 10 | 27 | 53 | 90 |
| 89 | James Philipo Musalika | Me | CCM | Nyang'hwale | 27 | 39 | 24 | 90 |
| 90 | Margreth Agness Mkanga | Ke | CCM | Hana | 20 | 14 | 56 | 90 |
| 91 | Hassan Chande Kigwalilo | Me | CCM | Liwale | 26 | 31 | 32 | 89 |
| 92 | Dr. Ali Tarab Ali | Me | CUF | Konde | 17 | 27 | 45 | 89 |
| 93 | Janeth Mourice Massaburi | Ke | CCM | Hana | 17 | 12 | 58 | 87 |
| 94 | Teddy Louise Kasella-Bantu | Ke | CCM | Bukene | 11 | 25 | 50 | 86 |
| 95 | Dr. Charles Ogesa F. Mlingwa | Me | CCM | Shinyanga Mjini | 11 | 15 | 59 | 85 |
| 96 | Mwinchoum Abdulrahman Idd Msomi | Me | CCM | Kigamboni | 21 | 14 | 50 | 85 |
| 97 | Maria Ibeshi Hewa | Ke | CCM | Hana | 17 | 18 | 49 | 84 |
| 98 | Juma Abdallah Njwayo | Me | CCM | Tandahimba | 18 | 23 | 43 | 84 |
| 99 | Felister Aloyce Bura | Ke | CCM | Hana | 10 | 18 | 55 | 83 |

| Nafasi | Jina | Jinsia | Chama | Jimbo | Maswali ya msingi | Maswali ya nyongeza | Michango | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 100 | Christopher Olonyokie Ole-Sendeka | Me | CCM | Simanjiro | 4 | 17 | 62 | 83 |
| 101 | Stephen Jones Galinoma | Me | CCM | Kalenga | 22 | 15 | 44 | 81 |
| 102 | Jackson Muvangila Makwetta | Me | CCM | Njombe Kaskazini | 17 | 27 | 36 | 80 |
| 103 | Amb.  Getrude Ibengwe Mongella | Ke | CCM | Ukerewe | 0 | 22 | 58 | 80 |
| 104 | Ludovick John Mwananzila | Me | CCM | Kalambo | 15 | 23 | 42 | 80 |
| 105 | Aziza Sleyum Ally | Ke | CCM | Hana | 17 | 16 | 46 | 79 |
| 106 | Manju Salum Omar Msambya | Me | CCM | Kigoma South | 0 | 32 | 47 | 79 |
| 107 | Dr. Zainab Amir Gama | Ke | CCM | Kibaha | 7 | 26 | 45 | 78 |
| 108 | Ernest Gakeya Mabina | Me | CCM | Geita | 23 | 35 | 20 | 78 |
| 109 | Janet Bina Kahama | Ke | CCM | Hana | 24 | 23 | 30 | 77 |
| 110 | Cynthia Hilda Ngoye | Ke | CCM | Hana | 14 | 26 | 37 | 77 |
| 111 | Estherina Julio Kilasi | Ke | CCM | Mbarali | 8 | 22 | 46 | 76 |
| 112 | Ali Khamis Seif | Me | CUF | Mkoani | 10 | 11 | 55 | 76 |
| 113 | Rosemary Kasimbi Kirigini | Ke | CCM | Hana | 17 | 20 | 39 | 76 |
| 114 | Suleiman Omar Kumchaya | Me | CCM | Lulindi | 16 | 19 | 41 | 76 |
| 115 | Martha Jachi Umbulla | Ke | CCM | Hana | 20 | 24 | 32 | 76 |
| 116 | Dr. Festus Bulugu Limbu | Me | CCM | Magu | 20 | 21 | 35 | 76 |
| 117 | Capt. John Damiano Komba | Me | CCM | Mbinga Magharibi | 18 | 27 | 31 | 76 |
| 118 | Grace Sindato Kiwelu | Ke | CHADEMA | Hana | 11 | 24 | 40 | 75 |
| 119 | Athumani Saidi Janguo | Me | CCM | Kisarawe | 9 | 14 | 52 | 75 |
| 120 | Mossy Suleiman Mussa | Me | CCM | Mfenesini | 32 | 17 | 26 | 75 |
| 121 | Ambassador Abdi Hassan Mshangama | Me | CCM | Lushoto | 24 | 11 | 40 | 75 |
| 122 | Haroub Said Masoud | Me | CCM | Koani | 16 | 35 | 24 | 75 |
| 123 | Wilson Mutagaywa Masilingi | Me | CCM | Muleba South | 6 | 9 | 60 | 75 |
| 124 | Masoud Abdallah Salim | Me | CUF | Mtambile | 17 | 12 | 45 | 74 |
| 125 | Kaika Saning'o Telele | Me | CCM | Ngorongoro | 16 | 29 | 29 | 74 |
| 126 | Frederick Mwita Werema | Me | CCM | Ex-officio Member | 0 | 0 | 73 | 73 |
| 127 | Prof. Philemon Mikol Sarungi | Me | CCM | Rorya | 9 | 7 | 57 | 73 |
| 128 | Hasnain Gulamabbas Dewji | Me | CCM | Kilwa Kusini | 23 | 23 | 26 | 72 |
| 129 | Bakari Shamis Faki | Me | CUF | Ole | 24 | 15 | 33 | 72 |
| 130 | Ameir Ali Ameir | Me | CCM | Fuoni | 11 | 5 | 56 | 72 |
| 131 | Beatrice Matumbo Shellukindo | Ke | CCM | Kilindi | 6 | 12 | 54 | 72 |
| 132 | Dorah Herial Mushi | Ke | CCM | Hana | 15 | 12 | 45 | 72 |
| 133 | Juma Said Omar | Me | CUF | Mtambwe | 12 | 7 | 53 | 72 |

| Nafasi | Jina | Jinsia | Chama | Jimbo | Maswali ya msingi | Maswali ya nyongeza | Michango | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 134 | Gaudence Cassian Kayombo | Ke | CCM | Mbinga Mashariki | 12 | 17 | 42 | 71 |
| 135 | Ramadhani Athumani Maneno | Me | CCM | Chalinze | 14 | 27 | 30 | 71 |
| 136 | Ephraim Nehemia Madeje | Me | CCM | Dodoma Mjini | 18 | 19 | 34 | 71 |
| 137 | Mohammed Rajab Soud | Me | CCM | Jang'ombe | 13 | 32 | 25 | 70 |
| 138 | Hemed Mohammed Hemed | Me | CUF | Chonga | 4 | 1 | 65 | 70 |
| 139 | Yahya Kassim Issa | Me | CCM | Chwaka | 20 | 40 | 10 | 70 |
| 140 | Hamza Abdallah Mwenegoha | Me | CCM | Morogoro Kusini | 9 | 9 | 51 | 69 |
| 141 | Khadija Salum Ally Al-Qassmy | Ke | CUF | Hana | 2 | 3 | 64 | 69 |
| 142 | Mtutura Abdallah Mtutura | Me | CCM | Tunduru | 10 | 18 | 40 | 68 |
| 143 | Mzee Ngwali Zubeir | Me | CCM | Mkwajuni | 25 | 34 | 9 | 68 |
| 144 | Dr. Juma Alifa Ngasongwa | Me | CCM | Ulanga Magharibi | 0 | 2 | 66 | 68 |
| 145 | Lediana Mafuru Mng'ong'o | Ke | CCM | Hana | 6 | 31 | 30 | 67 |
| 146 | Damas Pascal Nakei | Me | CCM | Babati Magharibi | 20 | 15 | 32 | 67 |
| 147 | Abdul Jabiri Marombwa | Me | CCM | Kibiti | 14 | 12 | 41 | 67 |
| 148 | Basil Pesambili Mramba | Me | CCM | Rombo | 7 | 10 | 48 | 65 |
| 149 | Idd Mohamed Azzan | Me | CCM | Kinonndoni | 6 | 12 | 46 | 64 |
| 150 | Richard Mganga Ndassa | Me | CCM | Sumve | 18 | 13 | 33 | 64 |
| 151 | Devota Mkuwa Likokola | Ke | CCM | Hana | 13 | 24 | 27 | 64 |
| 152 | John Samwel Malecela | Me | CCM | Mtera | 1 | 44 | 19 | 64 |
| 153 | Laus Omar Mhina | Me | CCM | Korogwe Vijijini | 25 | 13 | 26 | 64 |
| 154 | Dr. Abdallah Omar Kigoda | Me | CCM | Handeni | 12 | 10 | 42 | 64 |
| 155 | Said Juma Nkumba | Me | CCM | Sikonge | 18 | 24 | 21 | 63 |
| 156 | Philemon Ndesamburo | Me | CHADEMA | Moshi Mjini | 19 | 17 | 26 | 62 |
| 157 | Shally Josepha Raymond | Ke | CCM | Hana | 6 | 14 | 42 | 62 |
| 158 | Charles Muguta Kajege | Me | CCM | Mwibara | 9 | 7 | 46 | 62 |
| 159 | Fatma Mussa Maghimbi | Ke | CUF | ChakeChake | 23 | 15 | 24 | 62 |
| 160 | Zuleikha Yunus Haji | Ke | CCM | Hana | 14 | 10 | 37 | 61 |
| 161 | Ibrahim Mohamed Sanya | Me | CUF | MjiMkongwe | 12 | 19 | 30 | 61 |
| 162 | Charles Mwera Nyanguru | Me | CHADEMA | Tarime | 8 | 7 | 46 | 61 |
| 163 | Lazaro Samuel Nyalandu | Me | CCM | Singida North | 16 | 24 | 20 | 60 |
| 164 | Bernadeta Kasabago Mushashu | Ke | CCM | Hana | 6 | 6 | 48 | 60 |
| 165 | Zakia Hamdani Meghji | Ke | CCM | Hana | 0 | 0 | 59 | 59 |
| 166 | Maida Hamad Abdallah | Ke | CCM | Hana | 14 | 9 | 36 | 59 |
| 167 | Dunstan Daniel Mkapa | Me | CCM | Nanyumbu | 20 | 19 | 19 | 58 |
| 168 | Benito William Malangalila | Me | CCM | Mufindi Kusini | 15 | 13 | 29 | 57 |

| Nafasi | Jina | Jinsia | Chama | Jimbo | Maswali ya msingi | Maswali ya nyongeza | Michango | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 169 | Luhaga Joelson Mpina | Me | CCM | Kisesa | 9 | 11 | 37 | 57 |
| 170 | Fred Mpendazoe Tungu | Me | CCM | Kishapu | 17 | 11 | 29 | 57 |
| 171 | Anna Richard Lupembe | Ke | CCM | Hana | 13 | 18 | 26 | 57 |
| 172 | Mariam Reuben Kasembe | Ke | CCM | Hana | 17 | 16 | 23 | 56 |
| 173 | Dr. Ibrahim Said Msabaha | Me | CCM | Kibaha Vijijini | 3 | 2 | 50 | 55 |
| 174 | Eliatta Nandumpe Switi | Ke | CCM | Hana | 7 | 16 | 32 | 55 |
| 175 | Anna Maulidah Komu | Ke | CHADEMA | Hana | 6 | 8 | 40 | 54 |
| 176 | Anastazia James Wambura | Ke | CCM | Hana | 7 | 5 | 41 | 53 |
| 177 | Dr. Omari Mzeru Nibuka | Me | CCM | Morogoro Mjini | 8 | 8 | 37 | 53 |
| 178 | Mariam Salum Mfaki | Ke | CCM | Hana | 6 | 7 | 37 | 50 |
| 179 | Mudhihir Mohamed Mudhihir | Me | CCM | Mchinga | 0 | 18 | 31 | 49 |
| 180 | Elizabeth nkunda Batenga | Ke | CCM | Hana | 4 | 17 | 27 | 48 |
| 181 | Parmukh Singh Hoogan | Me | CCM | Kikwajuni | 23 | 18 | 7 | 48 |
| 182 | Meryce Mussa Emmanuel | Ke | CUF | Hana | 5 | 15 | 28 | 48 |
| 183 | Dr. Anthony Mwandu Diallo | Me | CCM | Ilemela | 0 | 4 | 43 | 47 |
| 184 | Omar Ali Mzee | Me | CUF | Kiwani | 11 | 7 | 29 | 47 |
| 185 | Lucy Thomas Mayenga | Ke | CCM | Hana | 11 | 14 | 21 | 46 |
| 186 | Brg. Gen. Hassan Athumani Ngwilizi | Me | CCM | Mlalo | 5 | 5 | 36 | 46 |
| 187 | Kilontsi Muhama Mporogomyi | Me | CCM | Kasulu Magharibi | 10 | 8 | 28 | 46 |
| 188 | Abubakar Khamis Bakary | Me | CUF | Hana | 5 | 9 | 31 | 45 |
| 189 | Kidawa Hamid Salehe | Ke | CCM | Hana | 13 | 11 | 21 | 45 |
| 190 | Tatu Musa Ntimizi | Ke | CCM | Igalula | 8 | 6 | 30 | 44 |
| 191 | Ahmed Ally Salum | Me | CCM | Solwa | 12 | 17 | 15 | 44 |
| 192 | Nazir Mustafa Karamagi | Me | CCM | Bukoba Vijijini | 0 | 1 | 42 | 43 |
| 193 | Josephine Johnson Genzabuke | Ke | CCM | Hana | 9 | 19 | 14 | 42 |
| 194 | Ali Said Salim | Me | CUF | Ziwani | 14 | 19 | 8 | 41 |
| 195 | Abdulkarim Esmail Hassan Shah | Me | CCM | Mafia | 5 | 16 | 20 | 41 |
| 196 | Eustace Osler Katagira | Me | CCM | Kyerwa | 0 | 0 | 41 | 41 |
| 197 | Feteh Saad Mgeni | Me | CCM | Bumbwini | 8 | 10 | 23 | 41 |
| 198 | Dr. Haji Mwita Haji | Me | CCM | Muyuni | 8 | 9 | 23 | 40 |
| 199 | Mohamed Said Sinani | Me | CCM | Mtwara Mjini | 14 | 9 | 17 | 40 |
| 200 | Ussi Ame Pandu | Me | CCM | Mtoni | 11 | 7 | 22 | 40 |
| 201 | Prof. Feethan Philipo Banyikwa | Me | CCM | Ngara | 16 | 3 | 20 | 39 |
| 202 | Kheri Khatib Ameir | Me | CCM | Matemwe | 9 | 7 | 23 | 39 |

| Nafasi | Jina | Jinsia | Chama | Jimbo | Maswali ya msingi | Maswali ya nyongeza | Michango | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 203 | Elisa David Mollel | Me | CCM | Arumeru Magharibi | 11 | 7 | 19 | 37 |
| 204 | Benedict Ngalama Ole-Nangoro | Me | CCM | Kiteto | 3 | 4 | 29 | 36 |
| 205 | Harith Bakari Mwapachu | Me | CCM | Tanga | 0 | 0 | 36 | 36 |
| 206 | Joseph James Mungai | Me | CCM | Mufindi Kaskazini | 0 | 2 | 34 | 36 |
| 207 | Ame Pandu Ame | Me | CCM | Nungwi | 14 | 9 | 12 | 35 |
| 208 | Fatma Abdulhabib Fereji | Ke | CUF | Hana | 6 | 5 | 22 | 33 |
| 209 | Florence Essa Kyendesya | Ke | CCM | Hana | 3 | 4 | 26 | 33 |
| 210 | Mwaka Abdulrahaman Ramadhan | Ke | CCM | Hana | 14 | 9 | 10 | 33 |
| 211 | Al-Shymaa John Kwegyir | Ke | CCM | Hana | 2 | 5 | 26 | 33 |
| 212 | Mohammed Amour Chombon | Me | CCM | Magomeni | 10 | 10 | 12 | 32 |
| 213 | Salim Abdallah Khalfan | Me | CUF | Tumbe | 8 | 5 | 18 | 31 |
| 214 | Riziki Said Lulida | Ke | CCM | Hana | 5 | 7 | 19 | 31 |
| 215 | John Magale Shibuda | Me | CCM | Maswa | 0 | 0 | 30 | 30 |
| 216 | Mwajuma Hassan Khamis | Ke | CUF | Hana | 5 | 0 | 24 | 29 |
| 217 | Haji Juma Sereweji | Me | CCM | Mwanakwerekwe | 6 | 8 | 15 | 29 |
| 218 | Abdisalaam Issa Khatib | Me | CCM | Makunduchi | 0 | 0 | 29 | 29 |
| 219 | Rita Louise Mlaki | Ke | CCM | Kawe | 2 | 8 | 18 | 28 |
| 220 | Ali Juma Haji | Me | CCM | Chaani | 4 | 3 | 21 | 28 |
| 221 | Fatma Othman Ali | Ke | CCM | Hana | 6 | 6 | 14 | 26 |
| 222 | Ahmed Mabkhut Shabiby | Me | CCM | Gairo | 6 | 5 | 15 | 26 |
| 223 | Rajab Ahmad Juma | Me | CCM | Tumbatu | 9 | 2 | 15 | 26 |
| 224 | Gideon Asimulike Cheyo | Me | CCM | Ileje | 0 | 0 | 25 | 25 |
| 225 | Abbas Zuberi Mtemvu | Me | CCM | Temeke | 0 | 2 | 23 | 25 |
| 226 | Issa Kassim Issa | Me | CCM | Mpendae | 5 | 5 | 15 | 25 |
| 227 | Dr. Rev. Getrude Rwakatare | Ke | CCM | Hana | 6 | 1 | 17 | 24 |
| 228 | Ismail Jussa Ladhu | Me | CUF | Hana | 0 | 5 | 19 | 24 |
| 229 | Halima Omar Kimbau | Ke | CCM | Hana | 0 | 4 | 20 | 24 |
| 230 | Edward Ngoyai Lowassa | Me | CCM | Monduli | 0 | 0 | 23 | 23 |
| 231 | Mohamed Ali Said | Me | CCM | Mgogoni | 12 | 1 | 10 | 23 |
| 232 | Kiumbwa Makame Mbaraka | Ke | CCM | Hana | 1 | 0 | 21 | 22 |
| 233 | Anna Margareth Abdallah | Ke | CCM | Hana | 0 | 1 | 21 | 22 |
| 234 | Nimrod Elirehema Mkono | Me | CCM | Musoma Vijijini | 1 | 1 | 19 | 21 |
| 235 | Bahati Ali Abeid | Ke | CCM | Hana | 4 | 4 | 13 | 21 |
| 236 | Samuel Mchele Chitalilo | Me | CCM | Buchosa | 7 | 1 | 13 | 21 |

| Nafasi | Jina | Jinsia | Chama | Jimbo | Maswali ya msingi | Maswali ya nyongeza | Michango | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 237 | Oscar Rwegasira Mukasa | Me | CCM | Biharamulo Magharibi | 3 | 9 | 8 | 20 |
| 238 | Joyce Martin Masunga | Ke | CCM | Hana | 1 | 2 | 15 | 18 |
| 239 | Zabein Muhaji Mhita | Me | CCM | Kondoa Kaskazini | 1 | 4 | 13 | 18 |
| 240 | Rev. Luckson Ndaga Mwanjale | Me | CCM | Mbeya Vijijini | 0 | 5 | 13 | 18 |
| 241 | Lolesia Jeremiah Bukwimba | Ke | CCM | Busanda | 3 | 3 | 11 | 17 |
| 242 | Asha Mshimba Jecha | Ke | CCM | Hana | 1 | 0 | 15 | 16 |
| 243 | Col. Saleh Ali Farrah | Me | CCM | Raha Leo | 3 | 3 | 9 | 15 |
| 244 | Mwanakhamis Kassim Said | Ke | CCM | Hana | 6 | 0 | 9 | 15 |
| 245 | Felix Christopher  Mrema | Me | CCM | Arusha | 0 | 0 | 15 | 15 |
| 246 | Joyce Nhamanilo Machimu | Ke | CCM | Hana | 2 | 1 | 12 | 15 |
| 247 | Sameer Ismail Lotto | Me | CCM | Morogoro -Kusini -Mashariki | 0 | 2 | 12 | 14 |
| 248 | Thomas Apson Mwang'onda | Me | CCM | Hana | 0 | 0 | 13 | 13 |
| 249 | Fatma Abdalla Tamim | Ke | CCM | Hana | 3 | 1 | 8 | 12 |
| 250 | Suleiman Ahmed Saddiq | Me | CCM | Mvomero | 0 | 2 | 9 | 11 |
| 251 | Ali Ameir Mohamed | Me | CCM | Donge | 5 | 3 | 3 | 11 |
| 252 | Salim Yussuf Mohamed | Me | CUF | Kojani | 0 | 0 | 11 | 11 |
| 253 | Hadija Saleh Ngozi | Ke | CCM | Hana | 2 | 0 | 9 | 11 |
| 254 | Mohammed Gulam Dewji | Me | CCM | Singida Mjini | 7 | 0 | 3 | 10 |
| 255 | Janeth Zebedayo Mbene | Ke | CCM | Hana | 0 | 1 | 9 | 10 |
| 256 | William Jonathan Kusila | Me | CCM | Bahi | 0 | 1 | 8 | 9 |
| 257 | Kingunge Ngombale-Mwiru | Me | CCM | Hana | 0 | 0 | 7 | 7 |
| 258 | Omar Sheha Mussa | Me | CCM | Chumbuni | 0 | 0 | 7 | 7 |
| 259 | Abdallah Salum Sumry | Me | CCM | Mpanda Magharibi | 0 | 0 | 7 | 7 |
| 260 | Juma Suleiman N'hunga | Me | CCM | Dole | 0 | 2 | 4 | 6 |
| 261 | Halima Mohammed Mamuya | Ke | CCM | Hana | 2 | 0 | 4 | 6 |
| 262 | Hassan Rajab Khatib | Me | CCM | Amani | 0 | 0 | 6 | 6 |
| 263 | Col.Lt. Yusufu Makamba | Me | CCM | Hana | 0 | 0 | 4 | 4 |
| 264 | Salum Khamis Salum | Me | CCM | Meatu | 0 | 0 | 4 | 4 |
| 265 | Ali Haji Ali | Me | CCM | Hana | 0 | 0 | 4 | 4 |
| 266 | Ali Haroon Suleiman | Me | CCM | Hana | 0 | 1 | 1 | 2 |
| 267 | Rostam Abdulrasul Aziz | Me | CCM | Igunga | 0 | 0 | 0 | 0 |

**Chanzo:** Tovuti ya Bunge la Tanzania (www.bunge.go.tz).

**Kiambatanisho na. 2: Nafasi ya ushiriki wa Wabunge (Wabunge wenye Nyadhifa za juu Serikalini)**

| Nafasi | Jina | Jinsia | Chama | Jimbo | Wadhifa | Maswali ya msingi | Maswali ya nyongesa | Michango | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Samuel John Sitta | Me | CCM | Urambo Mashariki | Spika | 0 | 0 | 829 | 829 |
| 2 | Anne Semamba Makinda | Ke | CCM | Njombe Kusini | Naibu spika | 0 | 0 | 682 | 682 |
| 3 | William Mganga Ngeleja | Me | CCM | Sengerema | Waziri | 3 | 7 | 166 | 176 |
| 4 | Stephen Masatu Wasira | Me | CCM | Bunda | Waziri | 0 | 0 | 165 | 165 |
| 5 | Prof. David Homeli Mwakyusa | Me | CCM | Rungwe Magharibi | Waziri | 0 | 0 | 144 | 144 |
| 6 | Prof. Jumanne Abdallah Maghembe | Me | CCM | Mwanga | Waziri | 0 | 0 | 143 | 143 |
| 7 | Dr. Mary Michael Nagu | Ke | CCM | Hanang | Waziri | 0 | 0 | 126 | 126 |
| 8 | Dr. Shukuru Jumanne Kawambwa | Me | CCM | Bagamoyo | Waziri | 0 | 0 | 119 | 119 |
| 9 | Prof. Mark James Mwandosya | Me | CCM | Rungwe Mashariki | Waziri | 0 | 0 | 118 | 118 |
| 10 | Shamsa Selengia Mwangunga | Ke | CCM | Hana | Waziri | 0 | 0 | 115 | 115 |
| 11 | Mustafa Haidi Mkulo | Me | CCM | Kilosa | Waziri | 0 | 0 | 112 | 112 |
| 12 | Philip Sang'ka Marmo | Me | CCM | Mbulu | Waziri | 0 | 0 | 109 | 109 |
| 13 | Dr.John Pombe Joseph Magufuli | Me | CCM | Biharamulo Mashariki | Waziri | 0 | 0 | 91 | 91 |
| 14 | Capt. John Zefania Chiligati | Me | CCM | Manyoni Mashariki | Waziri | 0 | 0 | 90 | 90 |
| 15 | Ezekiel Magolyo Maige | Me | CCM | Msalala | Naibu Waziri | 14 | 25 | 48 | 87 |
| 16 | Margaret Simwanza Sitta | Ke | CCM | Hana | Waziri | 0 | 0 | 83 | 83 |
| 17 | Lawrence Kego Masha | Me | CCM | Nyamagana | Waziri | 0 | 0 | 75 | 75 |
| 18 | Hawa Abdulrahman Ghasia | Ke | CCM | Mtwara Vijijini | Waziri | 0 | 0 | 74 | 74 |
| 19 | Aggrey Deaisile Joshua Mwanri | Me | CCM | Siha | Naibu Waziri | 15 | 13 | 40 | 68 |
| 20 | Prof. Juma Athuman Kapuya | Me | CCM | Urambo Magharibi | Waziri | 0 | 0 | 68 | 68 |
| 21 | Prof. Peter Mahamudu Msolla | Me | CCM | Kilolo | Waziri | 0 | 0 | 63 | 63 |
| 22 | Capt. George Huruma Mkuchika | Me | CCM | Newala | Waziri | 12 | 15 | 31 | 58 |
| 23 | Mwantumu Bakari Mahiza | Ke | CCM | Hana | Naibu Waziri | 0 | 0 | 57 | 57 |
| 24 | Mathias Meinrad Chikawe | Me | CCM | Nachingwea | Waziri | 0 | 0 | 52 | 52 |
| 25 | Bernard Kamillius Membe | Me | CCM | Mtama | Waziri | 0 | 0 | 49 | 49 |
| 26 | Omar Yussuf Mzee | Me | CCM | Kiembesamaki | Naibu Waziri | 0 | 0 | 49 | 49 |
| 27 | Christopher Kajoro Chiza | Me | CCM | Buyungu | Naibu Waziri | 0 | 0 | 49 | 49 |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 28 | Dr.Batildan Salha Burian | Ke | CCM | Hana | Waziri | 0 | 0 | 47 | 47 |
| 29 | Adam Kighoma Ali Malima | Me | CCM | Mkuranga | Naibu Waziri | 1 | 3 | 39 | 43 |
| 30 | Dr. Diodorus Buberwa Kamala | Me | CCM | Nkenge | Waziri | 0 | 0 | 42 | 42 |
| 31 | Mizengo Kayanza Peter Pinda | Me | CCM | Mpanda Mashariki | Waziri Mkuu | 0 | 0 | 40 | 40 |
| 32 | Dr. Aisha Omar Kigoda | Ke | CCM | Hana | Naibu Waziri | 0 | 0 | 38 | 38 |
| 33 | Dr. James Mnanka Wanyancha | Me | CCM | Serengeti | Naibu Waziri | 7 | 7 | 24 | 38 |
| 34 | Celina Ompeshi Kombani | Ke | CCM | Ulanga Mashariki | Waziri | 0 | 0 | 34 | 34 |
| 35 | Dr. Hussein Ali Mwinyi | Me | CCM | Kwahani | Waziri | 0 | 0 | 34 | 34 |
| 36 | Joel Nkaya Bendera | Me | CCM | Korogwe Mashariki | Naibu Waziri | 0 | 0 | 32 | 32 |
| 37 | Dr. Lucy Sawere Nkya | Ke | CCM | Hana | Naibu Waziri | 3 | 6 | 21 | 30 |
| 38 | Dr. Milton Makongoro Mahanga | Me | CCM | Ukonga | Naibu Waziri | 0 | 0 | 28 | 28 |
| 39 | Mohamed Aboud Mohamed | Me | CCM | Hana | Naibu Waziri | 0 | 0 | 27 | 27 |
| 40 | Sophia Mattayo Simba | Ke | CCM | Hana | Waziri | 0 | 0 | 27 | 27 |
| 41 | Dr. Cyril August Chami | Me | CCM | Moshi Vijijini | Naibu Waziri | 0 | 0 | 26 | 26 |
| 42 | Dr. David Mathayo David | Me | CCM | Same Magharibi | Naibu Waziri | 0 | 0 | 25 | 25 |
| 43 | Muhammed Seif Khatib | Me | CCM | Uzini | Waziri | 0 | 0 | 25 | 25 |
| 44 | Dr. Maua Abeid Daftari | Ke | CCM | Hana | Naibu Waziri | 0 | 0 | 24 | 24 |
| 45 | Gaudentia Mugosi Kabaka | Ke | CCM | Hana | Naibu Waziri | 0 | 0 | 23 | 23 |
| 46 | Ambassador Hamis Suedi Kagasheki | Me | CCM | Bukoba Mjini | Naibu Waziri | 0 | 0 | 20 | 20 |
| 47 | Dr. James Alex Msekela | Me | CCM | Tabora Kaskazini | Mkuu wa Mkoa | 0 | 0 | 19 | 19 |
| 48 | Hezekiah Ndahani Chibulunje | Me | CCM | Chilonwa | Naibu Waziri | 0 | 0 | 15 | 15 |
| 49 | Dr. Emmanuel John Nchimbi | Me | CCM | Songea Mjini | Naibu Waziri | 0 | 0 | 15 | 15 |
| 50 | Dr. Christine G. Ishengoma | Ke | CCM | Hana | Mkuu wa Mkoa | 0 | 0 | 13 | 13 |
| 51 | Mohammed Abdi Abdulaziz | Me | CCM | Lindi Mjini | Mkuu wa Mkoa | 0 | 0 | 13 | 13 |
| 52 | Jeremiah Solomon Sumari | Me | CCM | Arumeru Mashariki | Naibu Waziri | 0 | 0 | 10 | 10 |
| 53 | Ambassador Seif Ali Iddi | Me | CCM | Kitope | Naibu Waziri | 0 | 0 | 8 | 8 |
| 54 | William Vangimembe Lukuvi | Me | CCM | Isman | Mkuu wa Mkoa | 0 | 0 | 7 | 7 |
| 55 | Monica Ngezi Mbega | Me | CCM | Iringa Mjini | Mkuu wa Mkoa | 0 | 0 | 6 | 6 |

**Chanzo:** Tovuti ya Bunge la Tanzania (www.bunge.go.tz).